**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA ISHIRINI

## KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE

**15 JUNI, 2015**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

_______________________

## MKUTANO WA ISHIRINI

**KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE – TAREHE 15 JUNI, 2015**

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Bajeti juu ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2014 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2015/2016 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) juu ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2014 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA FEDHA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

## II. MASWALI:

### OFISI YA WAZIRI MKUU:

### 190. MHESHIMIWA RACHEL MASHISHANGA ROBERT (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Ukame unaoendelea kuikumba Mikoa ya Shinyanga na Simiyu unatishia upungufu mkubwa wa chakula:-

Je, Serikali inafanya jitihada gani kupeleka msaada wa chakula kwa wakati.

### 191. MHESHIMIWA DKT. AUGUSTINE LYATONGA MREMA (VUNJO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu :- Wako wafanyabiashara ambao walinyang'anywa Mahindi yao wakiwa katika vijiji vya Chekereni, Njiapanda, Himo, Marangu Mtoni na Mwika katika Jimbo la Vunjo wakidaiwa

kupeleka Mahindi hayo nchini Kenya wakati Jimbo la Vunjo halipakani na nchi ya Kenya:-

(a) Je, Serikali ilijuaje kuwa Mahindi hayo yalikuwa yakipelekwa Kenya wakati yalikuwa katika Jimbo la Vunjo;

(b) Je, ni Mahindi kiasi gani yenye thamani gani yalikamatwa ndani ya Jimbo la Vunjo na kurejeshwa kwa wananchi;

(c) Je, ni kiasi gani cha Mahindi kilitaifishwa na kuuzwa na Serikali na fedha hizo ziko wapi, zitarejeshwa lini kwa wahusika.

**OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):**

**192. MHESHIMIWA MARIAM REUBEN KASEMBE (MASASI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu):- Serikali imeweka Mpango Mzuri wa kuboresha utendaji kazi kupitia Mpango wa Matokeo Makubwa sasa (*BRN*):-

(a) Je, ni mafanikio gani yamepatikana mpaka sasa kutokana na mpango huo;

(b) Je, ni changamoto gani zimejitokeza katika utekelezaji wa mpango huo.

## WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

**193. MHESHIMIWA ROSWEETER FAUSTIN KASIKILA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Mikataba, Itifaki na Maazimio ya Kimataifa na Kikanda huwa kwenye Lugha ya Kiingereza hivyo wananchi wengi hushindwa kufanya rejea:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa Mikataba hiyo inatafsiriwa pia katika lugha ya Kiswahili.

## WIZARA YA MAJI:

**194. MHESHIMIWA JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Kwa sababu maji ni uhai:-

(a) Je, ni lini miradi ya maji katika vijiji kumi Bukoba Vijijini na kwingineko nchini itakamilika;

(b) Je, ni lini vijiji vingine ambavyo haviko kwenye mpango wa miradi hii ya vijiji kumi vitapata maji ili wananchi waondokane na adha ya ukosefu wa maji;

(c) Je, kwanini Serikali haitaki kuanzisha mfuko wa maji ili kutatua tatizo la maji nchini.

**195. MHESHIMIWA DKT. FESTUS BULUGU LIMBU (MAGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ahadi ya kuwapatia maji ya uhakika Wananchi wa Mji wa Magu imefikia wapi.

**WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

**196. MHESHIMIWA KHATIB SAID HAJI (KONDE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- Serikali kila mwaka imekuwa ikitoa vibali vya uingizaji sukari nchini kwa wafanyabiashara kwa lengo la kufidia upungufu unaotokana na uzalishaji mdogo wa sukari katika viwanda vyetu:-

(a) Je, ni kiasi gani cha sukari kinaingizwa nchini kufidia upungufu huo;

(b) Kutokana na kuondolewa kodi kwa bidhaa hiyo katika kipindi hicho; Je, ni unafuu gani wa bei anaoupata Mwananchi katika kipindi hicho.

## WIZARA YA UJENZI:

**197. MHESHIMIWA JUMA ABDALLAH NJWAYO (TANDAHIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Ujenzi:-
Barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala hadi Masasi imewekwa kweye Mpango wa Kufanyiwa Upembuzi Yakinifu kwa ajili ya Maandalizi ya kuwekwa lami kama inavyoonyeshwa kwenye Ilani ya CCM 2010:-

Je, upembuzi yakinifu wa Barabara hiyo umefikia Kiwango gani hadi sasa.

**198. MHESHIMIWA ASSUMPTER NSHUNJU MSHAMA (NKENGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-
Barabara ya kutoka Bunazi kuelekea Kikunyu kupitia Kagera Sugar ni muhimu kwa sababu inakwenda kiwanda cha Sukari Kagera na hutumiwa na magari makubwa yanayopeleka miwa kiwandani; lakini barabara hiyo inawapa shida Wakulima wanaopeleka miwa kiwandani kwa wenye magari kuwatoza bei kubwa kwa sababu ya ubovu wa barabara hiyo:-

(a) Je, ni lini Serikali itatengeneza kipande cha barabara kutoka Bunazi – Kagera Sugar;

(b) Je, Serikali kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita imeshatumia kiasi gani cha pesa kutengeneza barabara hiyo;

(c) Je, kwa nini kipande cha km 19 kisitengenezwe kwa lami kwa sababu kinapitisha tani milioni moja kupeleka bidhaa kiwandani na hivyo kufanya barabara hiyo kuharibika kila mara.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):**

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2014 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha, 2015/2016.

***(Majadiliano yanaendelea)***

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **DKT. T. D. KASHILILAH** |
| **15 JUNI, 2015** | **KATIBU WA BUNGE** |